## Maswali

1. Mungu alichugua kina nani kuwa watu wake?
2. Nabii wa Mungu Israeli alikuwa nani?
3. Mbona watu walitaka mfalme?
4. Mfalme wa kweli wa Israeli alikuwa nani?
5. Mfalme binadamu angefanya nini?
6. Mungu alichagua nani kuwa mfalme?
7. Mungu alionyeshaje kwamba amechagua Sauli?
8. Sauli alijisikiaje juu ya kazi mpya?
9. Sauli alipigana na nani? Mbona?
10. Samweli aliambia mfalme na watu wake nini?

## Majibu

1. Mungu alichagua Ibrahimu na familia yake kuwa watu wake.Wanaitwa taifa la Israeli.
2. Samweli alikuwa nabii wa Mungu katika Israeli.
3. Watu walitaka mfalme atakayeonekana mzuri ili wawe kama mataifa mengine.
4. Mfalme wa Israeli wa kweli alikuwa Mungu.
5. Mfalme binadamu angechukua wana, binti, mashamba, maavuno, mifugo na watumishi wao.
6. Mungu alichagua Sauli kuwa mfalme.
7. Mungu alichagua Sauli na akaonyesha kwa kumminia mafuta kichwani.Baadaye akamfanya kuwa mfalme mbele ya watu wote.
8. Sauli aliogopa kwamba hataweza kufanyo hiyo kazi mpya.
9. Sauli aliwapiga Waamoni kwa sababu walikuwa wakitisha watu wa Mungu.
10. Samweli aliwahatarisha Sauli pamoja na watu wote kwamba waendelee kuabudu Mungu pamoja,la sivyo wangekufa.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1 Mwaka wa 2**

# 12 Sauli afanywa mfalme

## Marejeo

1 Samweli 8 + 9

## Kiini cha somo

Haijalishi unaonekana vizuri namna gani,cha maana ni moyo wako

## Maneno maalum

1. Ibrahimu + taifa la Israeli + Samweli + amua + mtumishi
2. Samweli anakufa + wafalme + kataa Mungu
3. Mfalme + jeshi + mtumishi + watu wanalia + mfalme mwanadamu
4. Mfalme + vita + kama wengine + Samweli
5. Kishi + Benyamini + Sauli + sura nzuri + punda + Samweli
6. Chakula + kiti cha heshima
7. Mispa + Mungu alitoa watu Misri + kataa Mungu + Mfalme + Sauli
8. Waamoni + jeshi kubwa + mfalme

**12.1** Mungu alichagua Ibrahimu na familia yake kuwa watu wake. Aliwaahidi kwamba atakuwa nao kila wakati. Watoto wa Ibrahimu wakawa taifa la Israeli. Samweli alikuwa nabii wa Mungu katika Israeli. Alikuwa muamuzi tena mtumishi wa Mungu. Alizunguka katika Israeli akifunza watu maneno juu ya Mungu. Alitumia sheria za Mungu na kutatua shida za watu. Alikuwa mtawa lakini aliendelea kuwa mzee kwa hivyo hangeweza kumtumikia Mungu kwa mda.

**11.2** Nani angeongoza Waisraeli baada ya Samweli kukufa? Watu waliona mataifa mengine na wafalme wakuwaongoza. Walimwendea Samweli na kusema, "Wewe unaendelea kuwa mzee na watoto wako hawatakuwa viongozi wazuri. Tunataka mfalme kama mataifa mengine." Samweli alihuzunika sana. Aliomba Mungu akifikiri watu wamemkataa yeye. Mungu alimwambia, "Hawajakukataa wewe Samweli. Mimi ndimi mfalme wao. Wamenikataa mimi!Lakini wahatarishe watakavyofanyiwa na yule mfalme."

**12.3** Samweli aliwahatarisha kwamba huyo mfalme atachukua wana wenu kuwa wanajeshi wake. Atachukua binti wenu kumfanyia kazi. Atachukua mashamba yenu mazuri ya mizabibu awape watumishi wake. Atawatoza fungu la kumi la mifugo yenu. Mwishowe watu watalia wakitaka mzaada kwa sababu mfalme ako anawafilizisha. Lakini Samweli aliwahatarisha tena, "Mungu hatawasikiliza kwa sababu walichagua mfalme mwanadamu badala ya Mungu."

**12.4** Haya yote watu waliyasikia,lakini bado walitaka mfalme. Walitaka kiongozi ili waonekane vizuri vitani, tena awatawale wawe kama watu wengine wote. Samweli aliambia Mungu na Mungu akasema, "Wape mfalme!" Akawapa na kuwaruhuzu waende nyumbani.

**12.5** Kishi alikuwa mtu tajiri sana kwa kabila la Benyamini. Alikuwa na mwana aliyeitwa Sauli. Alikuwa mrefu na wa sura nzuri. Lakini Sauli hakumjua vizuri.Sauli na watumishi wake walikuwa wakitafuta punda zao. Mtumishi mmoja akasema, "Tungemuuliza nabii atusaidie." Kwa hivyo wakaenda kumuona. Samweli alikuwa amemsubiri mtu atakayekua mfalme kwa sababu Mungu alikuwa amemwambia kwamba atakuja kumuona hiyo siku.



**12.6** Samweli alichukua Sauli pamoja na watu wengine wa maana waende wakule chakula. Alimpa Sauli kiti cha heshima akalie.Kesho yake kwa siri, alimwambia Sauli kwamba atakuwa mfalme. Alimminia mafuta kichwani kuonyesha alikuwa amechaguliwa na Mungu. Sauli alipofika nyumbani, hakuambia mtu wa familia yake yeyote.

**12.7** Samweli aliita watu wote waje Mispa. Akawambia hivi, "Mungu alimtoa Misri,akamlinda na sasa mmemkataa. Mnataka mfalme! Sasa Mungu anawapa mfalme. "Wakati huo Sauli alikuwa amechificha. Aliogopa kwamba hataweza kazi mpya hiyo. Mungu alimwambia Samweli penye Sauli alikua amechificha. Wakaenda kumleta mbele ya kila mtu. Alionekana mwenye nguvu na mrefu.Watu walishangilia, "Mfalme na aishi milele!" Samweli aliawambia sheria za ufalme zote na kuziandika. Mwishowe watu wote walirudi nyumbani.

**12.8** Waamoni watu waovu walipanga kushambulia Waisraeli walioishi Yabeshi-Gileadi. Aliwaogofia kwa kuwambia eti atawatoa macho yao ya kuume. Sauli alikasirika sana aliposikia haya maneno. Akatumanisha habari Waisraeli waje wote. "Njoo na mnifwate." Jeshi kubwa lilikusanyika na kuwapiga Waamoni. Watu wote walifurahi kwa sababu Sauli alikuwa mfalme wao. Walikusanyika na kumfanya Sauli mfalme na kumsujudia Mungu. Samweli aliwahatarisha pamoja na mfalme wao kwamba waendelee kuabudu la sivyo wote na mfalme watakufa.